**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/LZ/2024/13**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000272**

**KATI YA**

**STEPHEN MTAKI KARIRO ............................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA............................................................ MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 28 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 28 mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa arekebishe usomaji wa dira uliokosewa na kutoa ankara isiyo sahihi ya mwezi Juni 2024 katika nyumba yake iliyopo Bweri, Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 27 Desemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 12 Februari 2025, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji. Mlalamikiwa ameifahamisha Mamlaka kwamba, baada ya kufuatilia usomaji wa dira yake kuanzia mwezi Juni 2024 mpaka Januari 2025 Mlalamikaji na Mlalamikiwa wamejiridhisha kwamba usomaji wa dira kwa sasa nyumbani kwa Mlalamikaji uko sawa. Baada ya kupokea utetezi kutoka kwa Mlalamikiwa, Mamlaka iliwasiliana na Mlalamikaji ili kutaka kufahamu kama ni kweli Mlalamikiwa ameshayafanyia kazi malalamiko yake kama alivyodai lakini Mlalamikaji hakua na uhakika. Kikao cha usuluhishi kilifanyika tarehe 24 Februari 2025, wakati wa kikao cha usuluhishi tulipitia ankara za Mlalamikaji na kujiridhisha kwa sasa ziko sahihi. Hivyo basi, Mlalamikaji ameridhika na ameomba kuondoa shauri lake EWURA kwa sababu muafaka umepatikana.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 28 mwezi Februari 2025.

...........................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**